
SANAD

# KUJIKINGA

## NGAO ZA WATU



Msururu wa kupotosha na kubadilisha

Sw

BARUA NAMBA 10 - MINYORORO NAMBA (114) 2018

Tabah Initiatives

**Kwa Jina la Mwenyezi Mungu mrehemevu mno na mwingi wa kurahamu.**

Kila jinsi ya sifa njema ni za Allah. Rehema na amani zimshukie Mtume wa Allah na jamaa zake na maswahaba wake na kila aliyemuunga.

## Ni kubwa zaidi kwa Allah kuliko kuangamia dunia nzima.

Baadhi ya vipote wenye misimamo mikali **vinatumia baadhi ya mas'ala ya kifiqihi ambayo wanazuoni wametofautiana, ili kufikia malengo ya kubomoa. Kupitia hayo wanahalalisha ya haramu na wanavunja matukufu. Katika uharamu mkubwa zaidi katika sheria ya Kiislamu ni uharamu wa kuuwa.**

**Kwani (utukufu wa damu) kama huu kuukosea ni vibaya zaidi kwa Allah kuliko kuangamia dunia nzima. Kama ilivyokuja kwenye hadithi tukufu: "Wallahi, hakika kuangamia dunia yote ni dogo kwa Allah kuliko kuuliwa muumini bila haki."**

**Pamoja na hili, hawa wenye misimamo mikali wanakhalifu misingi na malengo ya dini ambayo umma wameafikiana na maimamu wamekubaliana kuwa** : Asili katika (umwagaji) damu ni uharamu.

Imepokewa na Tirmidhi 1395 (Milango ya Fidia), an-Nasa'i 3987 (Mlango wa Kuharamisha Damu), Ibn Majah 2619 (Milango ya Fidia) na wengineo kutokamana na hadithi ya Ibn Umar.

Na katika mas'ala haya ambayo hivi vipote wenye misimamo mikali vimeyatumia kama hoja ya vitendo vyao vyenye kudhuru ni “Mas'ala ya Kujikinga” ambayo yametajwa katika vitabu vya Usul fiqhi na fiqhi.

Na yametumiwa mas'ala haya kwa malengo ya kuhalalisha kuuwa, kuripua, kuharibu na kubomoa bila kizuizi cha dini au huruma au tabia au ada.

Wanayapa mambo majina ambayo siyo kwa madai ya jihadi bila hoja katika dini ya Allah wala dalili kwenye Quran na Hadithi.

## Ni Nini Maana ya Kujikinga?

Ni adui wakati wa kupigana anapojikinga na ambao ni haramu kuwaua:

katika Waislamu

na ambao wako kwenye hukmu yao: kama Watu wa Kitabu na ambao wana ahadi ya amani au watoto.



Basi adui anawaweka mbele yake kama ngao ili ajikinge na mashambulizi ya Waislamu… yaani kama ngao ya watu.

## Hukmu ya Kujikinga Kutumia Watu

Mas'ala ya kuua wenye kukinga (ngao za watu) ambao ni Waislamu, wanazuoni wametofautiana. Kikundi katika wao wamesema haifai kwa sababu ya neno lake Allah aliyetukuka {Na lau si wanaume Waumini na wanawake Waumini msio wajua mkawasaga na mkaingia makosani kutokana nao bila ya kujua…} [Surat al-Fath:25].



- **Na katika maimamu waliosema hivo ni:**
  **Al-Awza'i, al-Layth , al-Qaffal , al-Baghawi na an-Nawawi .**

Na Imam al-Layth bin S'ad (Mungu amrehemu) amesema:
"Kuwacha kufungua ngome ambayo inawezekana kufunguliwa ni bora kuliko kuuwa Muislamu mmoja bila haki." Al-Mughni cha ibn Qudama (9/288).

Na baadhi ya maimamu wamesema inafaa kwa ajili ya kuangalia maslaha yaliyowachiliwa wazi ambayo yanafungamana na malengo na maslaha ya umma kwa jumla, na wameiwekea masharti na vidhibiti . Miongoni mwake ni:

---

2. Al-Mughni cha ibn Qudama (9/288)
3. Rawdha at-Talibin cha an-Nawawi (10/246)
4. Rawdha at-Talibin cha an-Nawawi (10/245)
5. Angalia Al-Mustasfa katika ilimu ya usul. cha Al-Ghazli (1/173)

## Masharti na Vidhibiti vya Kujikinga

Haifai kumuua Muislamu ambae maadui wamemtumia kama kinga na ngao yake ispokuwa kwa masharti. Miongoni mwake ni:



1. Maslaha yawe ni ya watu wote kwa jumla na sio kwa kipote kidogo.
2. Iwe wamejikinga nao hali ya kuwa Waislamu wako kwenye kupambana na makafiri katika vita.
3. Na maslaha yawe kwenye fitna ni ya hakika na sio kulingana na dhana.
4. Na iwe kuna dharura ambayo inawasonga Waislamu

Yasipopatikana masharti haya basi haifai kumuua. Ama maslaha yakiwa ni ya dharura na maafa yanarudi kwa umma wote, iwe ni baina kumalizwa waislamu au kubakia, basi dharura kama hii itafanya iwe inafaa, kwani itafanya wamalizwe yule aliyetumiwa kama kinga na Waislamu na Uislamu. Nayo itakuwa ni katika kuondoa madhara ya jumla kwa kufanya madhara khaswa. Na hili wanaafikiana wenye akili wote katika waislamu na wasiokuwa waislamu.

# Kukisia Kulio Batili Kwa Kila Namna

Je, inafaa kufananisha kulipuwa na kuuwa waso na makosa kwa kudai kufananisha na mas'ala ya kujikinga kwa kutumia watu ?

Jibu ni Hapana !

## Kufananisha Au Kukisia Ambako Ni Makosa :

Nako ni kufananisha pamoja na kuwa kuna tofauti, kwa sababu ya kutofautiana baina taswira ya kulipua na ya makafiri kujikinga kwa kutumia Waislamu, zinatofautiana kiasi cha kufanya kuwa haiwezekani kabisa kisheria kukisia mojawapo kwa nyingine. Kwani hakuna kinga wala mwenye kujikinga wala mateka ambae yuko mikononi mwa adui!!! Bali ni khiyana. Kwahio ni uadui tu. Wala haipatikani taswira ya kujikinga kwa kutumia watu, wala hata maana moja katika maana zinaz ozingatiwa kuhusiana nayo.

## Kuvuwa Kutokamana na Asili:

Asili katika (umwagaji) damu ni uharamu. Kuuwa waliotumiwa kama kinga imevuliwa kutokamana na asili, na kumetofautianwa kuhusu kufaa kwake, na waliojuzisha wameifunga kwa masharti. Kwahio haifai kabisa kukunjuka katika kuikisia!!

## Kutofautiana Sehemu na Zama :

Hii kujikinga ambayo imetofautianwa, haifai kuichukua kutoka kwenye uwanja wa vita na zama za vita za kizamani, na kuileta katika zama za sasa, kwa sababu sahii katika haya milipuo (ya mabomu) katika nchi za Waislamu au kwingine hakupatikani maadui ambao wamejificha nyuma ya waliotekwa nyara. Bali ambalo lipo kwa sasa ni kuwahifadhi waliotekwa nyara kwa malengo ya kubadilishana au mfano wa lengo hili, na sio kuwauwa!

Na asiekuwa mateka, kama ambae anaishi jirani na makafiri au mlinzi au mpita njia hachukui hukmu ya aliyetumiwa kama ngao, hata kwa ambao wamejuzisha hilo.

## Kujitetea Kunakokataliwa

Wenye misimamo mikali wanatetea kitendo chao hiki kwa kusema: "Tunafanya hilo ili kuwaudhi makafiri!!"

Na ni kinyume kabisa. Kwani kitendo kama hiki hutoa matokeo kama:



1. Huwaletea Waislamu kubomoka na kuvunjika!

2. Na inakuwa ndiyo njia ya adui kuwasaliti Waislamu, kuwafungia, kuchukua mali yao na kuharibu maslaha yao!

3. Kitendo chao si lingine ispokuwa ni kukusudia ufisadi katika ardhi na kuutia ulimwengu wote hamasa dhidi ya Waislamu na kuwabandikiza wao na ulinganizi wao jina la unyama na ugaidi!

## Kwahio

ni kujitetea kuliokataliwa, na inakhalifu kanuni za kielimu wakati wa kuzitumia hukmu za kisheria. Na katika hizo ni kanuni muhimu ambayo maimamu wameafikiana kuihusu.

### Kanuni muhimu

"Lau zitapingana maslaha na uharibifu basi itachungwa kuondosha uharibifu kuliko kuleta maslaha."

## Hoja Dhaifu

Hawa wenye kutumia mas'ala haya na kutoa fatwa na kuuwa Waislamu na kuwaripua wanatumia hoja kuwa: "Tunawaharikishia kuwaingiza peponi!"

Hakuna aliyewatangulia katika hili. Wala haijatajwa kwenye Quran wala Sunnah. Nayo ni kumzulia Mungu na Mtume. Bali kwa uhakika ni kuichezea dini na sheria na misingi yake iliyokita. Kwani ni nani aliyewapatia hakika ya kumaliza uhai wa Waislamu? Kwani huenda uhai wao ukawa ni ziada katika kheri kwao!

### Msimamo wa Quran Ambao Unaimaliza Fikra ya Makosa ya Wanaopingana na Mafunzo ya (Allah) Mola wa Viumbe

**Ni msimamo ambao umepatikana katika suluhu ya Hudaybiya, msimamo ambao Quran umeubakisha milele tena kwa uwazi kabisa, wakati Mungu alipowakataza Waislamu kuwauwa Maqureshi katika neno lake: {Na lau si wanaume Waumini na wanawake Waumini msio wajua mkawasaga na mkaingia makosani kutokana nao bila ya kujua... Mwenyezi Mungu (amefanya haya) ili amuingize amtakaye katika rehema yake. Lau wangelitengana bila ya shaka tungeliwaadhibu waliokufuru kwa adhabu chungu.} [Surat al-Fath:25].**

**{msio wajua} yaani msiowajua kama ni waumini**

**{mkawasaga} kwa kuwauwa na kuwavamia**

**Na maana yake ni kuwa: lau kwamba hamutowadhuru waumini wanaume na wanawake ambao hamuwajui basi Mungu angewaruhusu kuingia Makka na tungewasalitia juu yao, lakini tumewachunga wale ambao wako Makka na wameficha imani zao.**

**Na neno lake {na mkaingia makosani} yaani katika aibu, washirikina watasema wameuwa watu wa dini yao.**

**{Lau wangelitengana} yaani lau wangepambanukana, lau waumini wangetengana kutokamana na makafiri basi angewaadhibu makafiri kwa upanga...**

**Na hii aya ni dalili ya kumchunga kafiri sababu ya utukufu wa muumini.**

Angalia tafsiri ya al-Qurtubi (16/286) pamoja na mabadilisho.

Basi angalia hii bayana ya Quran na huu mfumo wa Mungu, vipi umekataza kupigana sababu ya kuwachunga waislamu ambao wanaficha imani zao na kwamba kitendo hiki kitawaletea waislamu aibu. Je, itakuwaje ambae yuwauwa waislamu waumini kwa kuwakusudia kusudi ?!

## Rehema ya Mungu
## Na angalizi la kidaawa

Kisha angalia hii rehema ya Mungu na angalizi la kidaawa katika neno lake aliyetukuka {ili amuingize amtakaye katika rehema yake} ambayo inafungua milango kwa ambao si waislamu waingie katika uislamu na kwenye rehema ya Mungu. Na hivi ndivyo alivyokuwa

Mtume katika miamala yake na makafiri, ana pupa nao, anawapa udhuru na anawaombea dua. Na hivi ndivyo anavyofaa kuwa kila muislamu, awe na pupa ya kuufikisha ubinadamu wote kheri.
Na utizame hii fikra bomofu ambayo inakhalifu yaliyoletwa na uislamu kutokamana na mafunzo mazuri, ambao wenye fikra hii huuwa na kuharibu sura ya uislamu na kuwafukuza mbali na uislamu, wanakhalifu misingi yote ya kiakili na ya kunakili.

## Ufupisho

1. Mas'ala ya kujikinga kwa kutumia watu ni mas'ala ya kifikra, wanazuoni wa usul na fiqhi wameyapigia mfano ili kuweka wazi baadhi ya maana za kanuni.

2. Wanazuoni wametofautiana katika mas'ala haya ya kujikinga, na wapo idadi ambao wamesema haifai, na aliyesema inafaa basi ameweka masharti na vidhibiti. Na maana yake hapa ni kuwa huu msimamo, nao ni adui anapojikinga na ambae ni haramu kumuuwa, ni wa kusongeka, muislamu hana khiyari yake katika hilo.

3. Kufananisha au kukisia kulipua na mas'ala ya kujikinga kwa kutumia watu ni makosa kwa kila upande, kwa sababu ya kutopatikana masharti ya kukisia, na kwa sababu kuua kinga ni kinyume na asili.

4. Ambalo limetokea katika suluhu ya Hudaybiya, na Qurani kutaja kuchelewa kuuwa sababu ya kuogopea waislamu wasidhurike zaidi ndani ya Makka, ni ushahidi mkubwa wa ubatili wa ambayo wanaitakidi hawa wabatilifu wavamiaji wakiukaji, wenye kuuwa waislamu na wa-siokuwa na hatia.

5. Fikra hii hainasibiani na malengo ya Uislamu wala haiuletei ispokuwa kuharibu sura yake iliyo nzuri samehevu, na kudhalilika ulinganifu wake duniani, kwa kuondosha msingi mkubwa wa Uislamu ambao ni huruma kwa ubinadamu wote na kuwa na pupa ya kuwaokoa na kuwaingiza katika dini ya Allah.


DAR AL FAQIH

مؤسسة طابة
Tabah Foundation
www.tabahfoundation.org

www.sanad.network
facebook.com/sanadnetwork
twitter: @sanadnetwork
youtube.com/sanadnetwork
instagram.com/sanadnetwork